



## KONGAMANO LA ISHIRINI NA MBILI LA KISWAHILI

**Bayreuth, tarehe 22 hadi tarehe 24 mwezi wa Mei 2009**

16 April 2009

Wapendwa Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Leo tunawaletea barua ya pili ya mwaliko ikiambatanishwa na ratiba yetu ya Kongamano. Mwaka huu tena, kongamano litafanyika siku tatu katika jengo la 'Iwalewa-House' (Münzgasse 9, tazama ramani kwenye ukurasa wa pili). Kongamano litaanza **Ijumaa tarahe 22 Mei** kuanzia **saa mbili na nusu asubuhi**. Kutakuwa na malipo ya usajili ya €6 kwa wasio wanafunzi na €3 kwa wanafunzi.

Wale watakaoandika makala yao kwa Kijerumani au Kiswahili itabidi waandike kifupisho cha makala kwa Kiingereza. Tena tunawaomba wote wanaoandaa makala zinazohusu lugha ya mdomo ('orality'), na watuletee kifupisho kwa Kiingereza (cha takribani nusu ya ukurasa), kwa sababu tunapanga tuwe na majadiliano makubwa kuhusu mada hiyo siku ya Jumamosi. Kifupisho kiletwe mapema kama iwezekanavyo kwa [swahili@uni-bayreuth.de](mailto:swahili@uni-bayreuth.de) (siku ya mwisho iwe **tarehe 15**, mwezi wa tano).

Kwa sababu mara hii makala tulizozipokea ni nyingi mno muda wa kutoa makala utakuwa **dakika 20** na **dakika 5** za kujadili kila wasilisho la makala. Tena kwa siku ya Ijumaa na siku ya Jumapili, tumepanga makala mbili ziwasilishwe wakati mmoja.

Mwaka huu, siku ya Jumamosi, tutakuwa na hafla nyingine maalum kwa ukumbusho wa mzee wetu, mwalimu wetu marehemu Sheikh Yahya Ali Omar, itakayoandaliwa na wenzetu kutoka SOAS (London).

Kabla Kongamano la Kiswahili halijaanza, wageni na wenyeji wote wanaombwa wakutane pamoja tarehe **21 Mei, saa moja jioni** katika mkahawa unaoitwa '**Delphi**' uliopo katika Badstr. 14 (tazama ramani). Huko kutakuwa na chakula na vinywaji ambavyo watakaohudhuria watajinunulia wao wenyewe.

Karibuni sana Bayreuth.

Wenu wakweli,

Prof. Gabriele Sommer, Clarissa Vierke M.A.,  
Afrikanistik I  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553556  
Fax.: +49-921-553627

Prof. Said A. M. Khamis  
Literaturen in afrikanischen Sprachen  
Universität Bayreuth,  
95440 Bayreuth  
Tel.: +49-921-553598  
Fax.: +49-921-553641

